MWONGOZO WA SHUGHULI ZA UFUGAJI NYUKI KATIKA MAPORI YA AKIBA, MAPORI TENGEFU NA ARDHIOEVU WA MWAKA 2021

_____

SEHEMU YA KWANZA

1.1 Utangulizi:

Ibara ya 27(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inampa kila mtu wajibu wa kulinda maliasilia zote za nchi. Aidha, Ibara ya 9(c) ya Katiba inaruhusu rasilimali za nchi kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote. Kutokana na msingi huo wa kikatiba, Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 inalenga kuhakikisha kuwa kuna uhifadhi endelevu wa rasilimali za wanyamapori na ardhioevu. Katika kufikia lengo hilo, Sera inahimiza uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori bila kuathiri mazingira kwa madhumuni ya kukabiliana na umasikini. Katika kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Sera inasisitiza, pamoja na mambo mengine, kuongeza uzalishaji katika sekta nyingine za kiuchumi.

Sera ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 inasisitiza kuwepo kwa makubaliano kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania na vikundi vya wafugaji wa nyuki yanayoruhusu ufugaji nyuki katika maeneo yaliyohifadhiwa. Sera hiyo inaelekeza kuwepo kwa uratibu wa pamoja kati ya Mamlaka na taasisi inayohusika na usimamizi wa ufugaji nyuki kwa masuala yanayohusu ufugaji nyuki katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Kwa mujibu wa Sera hiyo, makubaliano kati ya Mamlaka na vikundi vya wafugaji nyuki ni mkakati wa kuhakikisha kuwa kuna uhifadhi endelevu kupitia ushiriki wa wananchi katika kusimamia na kutumia maliasilia za nchi. Vilevile, Sera inaainisha kuwepo kwa utaratibu wa kugawana faida kati ya Mamlaka na wafugaji wa nyuki wanaofuga katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Vilevile,kifungu cha 8 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Na 5 ya mwaka 2009 inampa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa TAWA ambaye ni Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA (CC) kuandaa miongozo ambayo itaiwezesha TAWA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Pamoja na kuwepo kwa matamko ya kisera yanayohusu kufanyika kwa shughuli za ufugaji nyuki katika maeneo yaliyohifadhiwa, Mamlaka haikuwa na mwongozo mahsusi wa shughuli za ufugaji nyuki katika maeneo ya Mamlaka. Kutokana na hali hiyo, shughuli hizo zimekuwa zikifanyika bila kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori ingawa kumekuwa na jitihada za kiutawala za kudhibiti na kusimamia shughuli hizo katika maeneo hayo. Kufanyika kwa shughuli hizo bila ya kuwepo kwa mwongozo mahsusi kumesababisha kuwepo kwa changamoto zinazoathiri uhifadhi wa wanyamapori na mazingira pamoja na kuikosesha Serikali mapato.

1.2 Madhumuni ya Mwongozo:

Mwongozo wa Shughuli za Ufugaji nyuki katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu wa mwaka 2021 unalenga kuweka utaratibu mahsusi wa usimamizi na uendeshaji wa shughuli hizo katika maeneo hayo. Kimsingi, Mwongozo unaweka masharti yanayohakikisha kuwa shughuli za ufugaji nyuki katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu zinafanyika bila kuathiri misingi ya uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori.

Baadhi ya masuala ambayo yanawekewa miongozo katika Mwongozo huu ni pamoja na utoaji wa vibali vya ufugaji nyuki, muda wa kuingia na kutoka katika maeneo ya hifadhi, zana na njia zinazoruhusiwa kutumika katika ufugaji nyuki na wajibu wa jumla wa mfugaji nyuki anayefanya shughuli zake katika eneo la hifadhi. Vilevile, Mwongozo unaainisha tozo mbalimbali ambazo Mamlaka itatoza katika kusimamia shughuli za ufugaji nyuki katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu.

1.3 Walengwa wa Mwongozo:

Maudhui ya Mwongozo huu yanawalenga wadau wa ufugaji nyuki wanaofuga katika katika mapori ya akiba, mapori tengefu na ardhioevu. Aidha, walengwa wengine wa Mwongozo huu ni pamoja na maafisa wanaoshughulika na uhifadhi, wataalam wa ufugaji nyuki na watafiti.

SEHEMU YA PILI

2.1 Mwongozo wa Shughuli za Ufugaji nyuki:

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, Mwongozo unakusudia kuainisha masharti ambayo yatazingatiwa na watu wanaokusudia kufanya shughuli za ufugaji nyuki katika maeneo yaliyo chini ya usimamizi wa Mamlaka. Masharti hayo ni:

2.1.1 Masharti ya Utoaji Kibali cha Ufugaji nyuki

(a) Mamlaka inaweza kutoa kibali cha kufanya shughuli za ufugaji nyuki katika eneo lililo chini ya usimamizi wake kwa wakazi wa eneo husika tu na endapo mwombaji wa kibali atakuwa ni:
   (i) mwanachama wa Chama cha Ushirika cha Wafugaji Nyuki kilicho karibu na eneo la hifadhi husika na kilichosajiliwa;
   (ii) kampuni ya kitanzania ambayo moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa kampuni hiyo ni ufugaji nyuki. Kampuni itatakiwa kuwasilisha nyaraka za kampuni *(Memorandum and Articles of Association)* ikiwa ni pamoja na cheti cha usajili;

(b) Kibali cha kufanya shughuli za ufugaji nyuki katika eneo lililo chini ya Mamlaka kinaweza kutolewa baada ya mwombaji kufanya yafuatayo:
   (i) kujaza Fomu ya Maombi ya Kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu;
   (ii) kulipa ada ya fomu ya maombi ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu ambayo haitarudishwa;
   (iii) kudhaminiwa na Chama cha Ushirika cha Wafugaji Nyuki ambacho kimesajiliwa kwa mwombaji ambaye si kampuni;
   (iv) kulipa ada ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu ambayo itatozwa kulingana na idadi ya mizinga; na
   (v) kuridhia kwamba TAWA haitakuwa na wajibu wowote kwa madhara yoyote yatakayompata akiwa katika eneo la hifadhi.

(c) Kibali cha Ufugaji nyuki kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(d) Kibali cha Ufugaji Nyuki kitakuwa cha kipindi cha miezi kumi na mbili;

(e) Mamlaka inaweza kuweka idadi maalum ya mizinga ambayo kila mfugaji atatakiwa kuwa nayo katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ufugaji nyuki.

(f) Mamlaka haitatoa Kibali cha Ufugaji Nyuki kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania au kampuni ambayo wanahisa wake si raia wa Tanzania;

(g) Mfugaji nyuki atatakiwa kuwa na Kibali cha Ufugaji Nyuki wakati wote anapokuwa katika eneo la hifadhi.

2.1.2 Masharti Kuhusu Mizinga ya Nyuki

(a) Mfugaji nyuki atatakiwa kutumia mizinga ya kisasa na zana za kisasa za urinaji wa asali;

(b) Mfugaji nyuki ataweka mizinga ya nyuki kwenye eneo lisilozidi kilomita kumi (10) kutoka kwenye mpaka wa hifadhi; na

(c) Mfugaji nyuki hataruhusiwa kuweka mizinga ya nyuki nje ya eneo lililotengwa na Mamlaka kwa madhumuni ya ufugaji nyuki.

2.1.3 Msimu wa Urinaji Asali

(a) Shughuli za urinaji asali katika eneo lililo chini ya Mamlaka zitafanyika kuanzia mwezi Aprili hadi Desemba;

(b) Mtu yeyote hatoruhusiwa kufanya shughuli za urinaji wa asali katika eneo lililo chini ya Mamlaka nje ya muda ulioainishwa kuwa ni msimu wa urinaji wa asali.

2.1.4 Taratibu za Kuingia katika Eneo la Hifadhi

(a) Mfugaji nyuki ataingia eneo la hifadhi kupitia maeneo yalioanishwa;

(b) Mfugaji nyuki hataruhusiwa kuingia katika eneo la hifadhi isipokuwa kupitia eneo lililoanishwa;

(c) Mfugaji nyuki atatakiwa kulipa ada ya kuingia katika eneo la hifadhi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu kila atakapokuwa anaingia katika eneo la hifadhi;

(d) Shughuli zinazohusu ufugaji nyuki zitafanyika katika eneo la hifadhi kuanzia saa mawio hadi machweo ya kila siku;

(e) Mfugaji nyuki hatatakiwa kuwepo ndani ya hifadhi baada ya machweo isipokuwa kwa kibali maalum cha Mamlaka.

2.1.5 Makambi ya Wafugaji Nyuki

(a) Mfugaji wa nyuki atakayeruhusiwa kwa kibali maalum kuwa ndani ya eneo la hifadhi baada ya machweo hataruhusiwa kujenga kambi ya kudumu katika eneo hilo;

(b) Kambi ya mfugaji nyuki itapaswa kuwa na maliwato ya muda iliyojengwa kwa kutumia nyasi, matete au makuti;

(c) Kambi ya mfugaji nyuki itajengwa katika eneo ambalo Mamlaka itaelekeza;

(d) Mfugaji nyuki atakayejenga kambi nje ya eneo lililoelekezwa na Mamlaka atatakiwa kuvunja kambi hiyo kwa gharama zake.

2.1.6 Zana za Urinaji Asali

(a) Shughuli za urinaji asali katika eneo la hifadhi zitaendeshwa kwa kutumia zana za kisasa;

(b) Matumizi ya moto hayataruhusiwa katika urinaji asali katika maeneo ya hifadhi.

2.1.7 Biashara ya Asali

(a) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingia katika eneo la hifadhi kwa madhumuni ya kununua asali isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa baada ya kulipa ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(b) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara yoyote isiyohusiana na asali katika eneo la hifadhi;

(c) Gari litakaloingia katika eneo la hifadhi kwa shughuli za ufugaji nyuki litatozwa ada ya kibali cha kuingia eneo la hifadhi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

2.1.9 Mwendokasi wa vyombo vya moto

Chombo cha moto kitakachoruhusiwa kuingia katika eneo la hifadhi hakitaruhusiwa kutembea mwendokasi unaozidi kilomita 50 kwa saa.

2.1.11 Wajibu Mahsusi wa Mfugaji Nyuki

Kila mfugaji nyuki mwenye kibali cha kufuga nyuki katika eneo la hifadhi atakuwa na wajibu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zote zinazohusu usimamizi wa maeneo ya hifadhi na masuala ya ufugaji nyuki. Katika kutimiza wajibu huo, mfugaji nyuki atakuwa na wajibu wa:

(a) kutoingilia maeneo ya malisho, mazalia au mapito ya wanyamapori;
(b) kutoingiza wanyama au ndege wafugwao katika eneo la hifadhi;
(c) kutoingiza au kutotumia ndani ya eneo la hifadhi vitu vya milipuko, sumu au kemikali ya aina yoyote;
(d) kutoingiza au kutotumia silaha ya aina yoyote isipokuwa ile iliyoruhusiwa katika Kibali;
(e) kutoingiza baiskeli ndani ya eneo la Mamlaka;
(f) kutoingiza pikipiki ndani ya eneo la Mamlaka;
(g) kutunza mazingira ya eneo la hifadhi;
(h) kutoharibu kwa namna yoyote uoto wa asili;
(i) kutoa taarifa kuhusu uhalifu wowote unotarajiwa kufanyika au ambao umefanyika katika eneo la hifadhi;

(j) kukabidhi kibali kilichojazwa taarifa husika (ikiwemo kiasi cha asali iliyopatikana) kwa afisa wa TAWA wakati wa kutoka eneo la hifadhi; na
(k) kuwasilisha kwa Mamlaka takwimu za ufugaji nyuki zinazoainisha, pamoja na mambo mengine, kiwango cha mazao ya ufugaji nyuki na mapato yaliyotokana na mazao hayo.

2.1.12 Utekelezaji wa Mwongozo:

(a) Utekelezaji wa Mwongozo huu utaanza baada ya kuidhinishwa na Kamishna wa Uhifadhi na kusambazwa kwa wadau katika tarehe itakayopangwa;

(b) Mtu aliyepewa kibali chini ya Mwongozo huu hataruhusiwa kuhamisha kibali hicho kwenda kwa mtu mwingine;

(c) Mtu yeyote atakayekiuka Mwongozo huu atafutiwa kibali kilichotolewa chini ya Mwongozo huu;

(d) Mtu atakayefutiwa kibali kilichotolewa chini ya Mwongozo huu hataruhusiwa kuomba kibali chochote kinachohusu shughuli za ufugaji wa nyuki hadi baada ya muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kufutiwa kibali.

SEHEMU YA TATU
HITIMISHO

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa maeneo ya hifadhi yanatumika kwa shughuli za ufugaji nyuki kwa manufaa ya wananchi bila kuathiri uhifadhi wa wanyamapori. Mwongozo huu endapo utatumika vyema utaimarisha uvunaji endelevu wa rasilimali hizo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Ni matumaini ya Mamlaka kuwa kila mdau anayehusika atazingatia Mwongozo huu katika shughuli za ufugaji nyuki zinazofanyika katika maeneo ya hifadhi. Kuzingatiwa kwa Mwongozo huu kunatarajiwa kuleta matokeo chanya katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka.

JEDWALI LA KWANZA

FOMU NA VIBALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UFUGAJI NYUKI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

JINA LA KITUO……

SEHEMU A (Ijazwe na Mwombaji wa Kibali):

Jina:…….

Namba ya Simu:……

Anwani ya Makazi:…….....

Eneo la Kufugia:……

Idadi ya Mizinga:……

Zana zitakazotumika…….

Sahihi:……..Tarehe:…….

SEHEMU B (Ijazwe na Chama cha Ushirika cha Wafugaji Nyuki):

Jina la Chama:……..

Jina la kikundi…….

Anwani ya Chama:……

Namba ya Usajili ya Chama:……...

Mamlaka iliyosajili Chama:……..

Maelezo ya Chama kuhusu mwombaji wa Kibali:

……..

Idadi ya mizinga ya mwombaji……

Sahihi ya Katibu wa Chama:……Tarehe:……..

PICHA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

KIBALI CHA UFUGAJI NYUKI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

JINA LA KITUO……

Kibali kimetolewa kwa:……(Jina)

Namba ya Simu:……

Anwani ya makazi:…….....

Eneo la Kufugia:……

Idadi ya Mizinga:……

Muda wa Kibali kuanzia:…….hadi:…….

Zana alizoruhusiwa……...

Ada iliyolipwa…… Namba ya malipo……..

Sahihi ya Mtoa Kibali…… Sahihi ya Mpewa Kibali……

Tarehe…… Tarehe…….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UFUGAJI NYUKI KATIKA MAENEO YALIYO CHINI YA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

JINA LA KITUO……

Jina la Kampuni……

Namba ya Usajili wa Kampuni……

Anwani ya Kampuni…….....

Namba ya Simu:……

Eneo la Kufugia:……

Idadi ya Mizinga:……

Zana zitakazotumika……

Sahihi:……..Tarehe:……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

KIBALI CHA UFUGAJI NYUKI KATIKA MAENEO YA HIFADHI

JINA LA KITUO……

Kibali kimetolewa kwa:…….(Jina la Kampuni)

Namba ya Usajili……

Anwani ya Kampuni:…….....

Namba ya Simu:……

Eneo la Kufugia:……

Idadi ya Mizinga:……

Muda wa Kibali kuanzia:…….hadi:…….

Zana zilizoruhusiwa……..

Ada iliyolipwa…… Namba ya malipo……..

Sahihi ya Mtoa Kibali…… Sahihi ya Mpewa Kibali……

Tarehe…… Tarehe…….

JEDWALI LA PILI

ADA MBALIMBALI

Na.	ADA		KIWANGO (TSH)	
			GCA	GRs
1.	Fomu ya Maombi ya Kibali cha Ufugaji wa Nyuki	Mtu binafsi	5000	5000
		Kampuni	10000	20000
2.	Kibali cha ufugaji nyuki	Mizinga isiyozidi 250	20,000	30,000
		mizinga 251 hadi 500	30,000	40,000
		Mizinga zaidi ya 500	40,000	50,000
3	Kibali cha mfugaji nyuki kuingia ndani ya hifadhi.		500 kwa siku	500 kwa siku
4.	Kibali cha kuingia katika eneo la hifadhi kwa madhumuni ya ununuzi wa asali		5000 kwa siku	10000 kwa siku
4.	Kibali cha baiskeli inayoingia katika eneo la Mamlaka kwa ajili ya kuchukua asali		200 kwa siku	200 kwa siku
5.	Kibali cha gari linaloingia katika eneo la hifadhi kwa ajili ya kuchukua asali:	chini ya tani 3	5000	10000
		kuanzia tani 3 hadi chini ya tani 7	10000	20000
		kuanzia tani 7 hadi tani 10	20000	50000